# UPELEKE ROHO YAKO

Mtunzi : Charles NYENZE
Maneno : Zaburi 103







1.Umsifu Bwana, ee roho yangu:
ndiwe mkubwa sana, ee Bwana, Mungu wangu.
Umevaa ungaro na utukufu,
umejivika mwanga kama vazi.

2.Umeweka dunia juu ya maweko yake:
haitasikitika milele na milele.
Uliifunika kwa kilindi kama kwa vazi,
maji yalisimama juu ya milima.

3.Umetokeza chemchemi zichururike mabondeni,
zitiririke kati ya milima.
Kandokando wanakaa ndege za angani,
wanatoa sauti kati ya matawi.

4. Unanywesha milima toka jumba lako,
dunia inashiba mazao ya matendo yako.
Unawaoteshea wanyama majani,
na mimea kwa matumizi ya wanadamu.

5.Kazi zako ni nyingi sana, ee Bwana
zote umezifanya kwa hekima.
Dunia imejaa viumbe vyako:
umsifu Bwana , ee roho yangu.